



**SWAHILI A1 – HIGHER LEVEL – PAPER 2**  
**SOUAHLÉLI A1 – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 2**  
**SUAHILI A1 – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 2**

Wednesday 16 May 2007 (morning)  
Mercredi 16 mai 2007 (matin)  
Miércoles 16 de mayo de 2007 (mañana)

2 hours / 2 heures / 2 horas

---

**INSTRUCTIONS TO CANDIDATES**

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Answer one essay question only. You must base your answer on at least two of the Part 3 works you have studied. You may include in your answer a discussion of a Part 2 work of the same genre if relevant. Answers which are not based on a discussion of at least two Part 3 works will not score high marks.
- You are not permitted to bring copies of the works you have studied into the examination room.

**INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS**

- N'ouvrez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Traitez un seul sujet de composition. Vous devez baser votre réponse sur au moins deux des œuvres de la 3<sup>e</sup> partie que vous avez étudiées. Le cas échéant, vous pouvez inclure dans votre réponse une discussion sur une œuvre du même genre littéraire étudiée dans la 2<sup>e</sup> partie du programme. Les réponses qui ne sont pas basées sur au moins deux des œuvres de la 3<sup>e</sup> partie n'obtiendront pas une note élevée.
- Vous n'êtes pas autorisé(e) à amener des exemplaires des œuvres que vous avez étudiées dans la salle d'examen.

**INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS**

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Elija un tema de redacción. Su respuesta deberá basarse en al menos dos de las obras estudiadas en la Parte 3. Se podrán hacer comentarios sobre una obra de la Parte 2 del mismo género, si fuera necesario. Las respuestas que no incluyan una discusión sobre al menos dos obras de la Parte 3 no recibirán notas altas.
- No se permite traer a la sala de examen copias de las obras estudiadas.

*Jibu swalii moja tu la insha. Jibu lako liegemee kwenye angalau kazi mbili za kazi ya sehemu ya 3 ulizojifunza. Unaweza kuingiza katika jibu lako majadiliano ya kazi ya sehemu ya 2 ya utanzu huohuo ambaa umejitayarisha nao. Majibu ambayo **hayana** mjadala wa angalau kazi mbili za sehemu ya 3 **hayatapewa** alama nydingi.*

### **Tamthilia**

#### **1. Ama**

- (a) Kwa kuzingatia kazi mbili ulizozisoma jadili jinsi waandishi wa kazi za fasihi wanavyoteua mazingira yao ya kisanaa na uonyeshe jinsi wanavyofaulu au kushindwa kutekeleza wajibu huu.

*Au*

- (b) Linganisha jinsi waandishi wengi wa tamthilia ulizozisoma wanavyoendeleza maswala ya usumbufu usiokuwa na matumaini na utupu wa kimaisha katika tamthilia zao.

### **Riwaya**

#### **2. Ama**

- (a) Ni kwa vipengele vipi waandishi katika kazi ulizozisoma wanavyoleta uhusiano kati ya mazingira na sifa za wahusika ili kuwapa wasomi nafasi ya kuelewa kazi zao barabara.

*Au*

- (b) Jadili ukitoa mifano kutoka kwa kazi ulizozisoma jinsi waandishi wengi wa riwaya wanavyochangia katika kuimarishe maadili katika jamii.

### **Ushairi**

#### **3. Ama**

- (a) Wasanii wengi wa ushairi wanatumia vipawa vyao vyaa ubunifu kuchangia katika maswala ya kimsingi yanayoikumba jamii. Jadili kauli hii huku ukirejelea angalau mashairi matatu uliyoyasoma kutoka kwa waandishi wawili au zaidi.

*Au*

- (b) Ni kwa kiasi kipi ushairi unavyoonekana kama kongamano la fani, maudhui na muktadha wa kijamii. Toa maoni yako huku ukirejelea kazi ulizojitayarishia.

## Riwaya ya mapenzi

### 4. Ama

- (a) Waandishi wengi hutumia mivutano na migogoro ya kijinsia kupitisha maoni yao kuhusu jamii. Linganisha uendelezaji wa mitafaruku hii ukizingatia kazi mbili au tatu ulizozisoma na uonyeshe unakubaliana na kauli hii kwa kiwango kipi.

*Au*

- (b) Kwa kuzingatia kazi mbili ulizozisoma toa maoni yako kuhusu waandishi uliowachagua na uonyeshe vile wanavyofanikisha kukuza na kutalii kipengele cha mapenzi.

## Maswali ya kijumla

### 5. Ama

- (a) Kwa kuzingatia kazi mbili au tatu ulizosoma linganisha jinsi swala la uadilifu linavyoendelezwa na uonyeshe umuhimu wake katika jamii.

*Au*

- (b) Utata katika fasihi mara nyingi huonekana kama kigezo cha kuboresha kazi za fasihi. Kwa kuzingatia angalau kazi mbili ulizozisoma talii swala hili na utoe maoni yako kuhusu vile utata huu unavyofanikisha au kukanganya katika kazi za fasihi.

*Au*

- (c) Jadili ukizingatia kazi mbili ulizozisoma jinsi waandishi wanavyotia chumvi maswala ya kawaida na kuyafanya yaonekane kama miujiza.

*Au*

- (d) Fasihi inawatetea kivipi wananchi wanaokandamizwa kisiasa. Jadili kauli hii huku ukirejelea kazi ulizozisoma.